# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**FEBRUARI, 2023**

# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2022 – 2023**

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote napenda kutumia fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mjuzi wa yote, Muumba na mwenye kurehemu kwa kutujaalia Afya njema iliyotuwezesha kukutana tena siku ya leo katika Baraza hili Tukufu kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu kwa mustakabali ulio bora. Aidha, namuomba Mwenyezi Mungu azidi kutuongoza ili tuweze kujadili mambo muhimu ya maendeleo ya Taifa letu na kutekeleza majukumu ya kazi za kuwatumikia wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** ninamshukuru tena Mwenyezi Mungu (SW) kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani, utulivu, umoja na mshikamano, hali ambayo imeendelea kuipa nafasi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wananchi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Napenda kuwasisitiza viongozi pamoja na wananchi kwa ujumla tuendelee kudumisha kikamilifu amani na utulivu tulionao kwani bila ya amani na utulivu hakuna maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa moyo wa dhati kabisa napenda kumpongeza na kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake, pia kujali kwake Utawala wa Sheria na Utawala Bora katika kipindi chote tokea ashike hatamu ya kuiongoza nchi yetu. Tunamuombea Mwenyezi Mungu azidi kumpa nguvu, imani na afya ili azidi kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha muhtasari wa Ripoti ya Kamati yetu ya

Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ripoti ambayo inaonesha shughuli zote ambazo tumezitekeleza katika kipindi hiki.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima, kupitia Ofisi zinazosimamiwa na Kamati yetu napenda kuelekeza salamu zangu za pongezi kwa Makamo wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamo wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah, Jaji Mkuu wa Zanzibar Mheshimiwa, Khamis Ramadhan Abdalla, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa juhudi na maarifa yao ya kumshauri ipasavyo Mheshimiwa Rais wetu hadi tukaweza kuyaona mafanikio yaliyofikiwa. Namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo huo na awajaalie maisha marefu yenye kheri na baraka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambayo imeundwa na kupewa majukumu kwa mujibu wa kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Kanuni ya 107 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la mwaka 2020. Aidha, majukumu ya Kamati hii, yameelezwa katika jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la Mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti hii inaakisi kazi za Kamati ambazo zimefanywa kuhusiana na utekelezaji wa Taasisi ambazo zipo chini yake kwa kipindi cha mwaka wa fedha, 2022/2023 na kwa kuzingatia Mipango mikuu ya Kitaifa ambayo inajumuisha Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 – 2025.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufuatilia utekelezaji wa kazi za kawaida na kazi za maendeleo, Kamati hii imekuwa ikizisimamia Taasisi kuu Tano za Serikali ambazo ni OR – Ikulu; Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais; Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi; OR – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora na OR – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ;.

**Mheshimiwa Spika,** Shukurani za pekee ziwaendee Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao makubwa ambayo yameiwezesha Kamati yetu kufanya kazi zake kwa ufanisi na uzoefu mkubwa na hatimae kukamilika kwa Ripoti hii. Napenda sasa niwatambue kwa majina Wajumbe wanaounda kamati hii kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii inafanyakazi na Makatibu wawili na Mkalimani wa lugha za alama mmoja ambao wamekuwa wakitusaidia kwa kiasi kikubwa na uweledi wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yetu, Msaada wa makatibu hao umekuwa ndio chanzo cha mafanikio makubwa ya Kamati hii. Makatibu hao ni:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Ali alawy Ali | Katibu |
| 2. | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| 3. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

## 2. MAUDHUI YA KAZI ZA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Katika sehemu hii, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeelezea kwa kina utekelezaji wa shughuli

zilizofanywa na Wizara ambazo zinasimamiwa na Kamati kwa kupokea taarifa tofauti za kila robo ya mwaka (quarterly reports) za utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara husika, kupokea taarifa za utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya mwaka uliopita, kukutana na wadau mbali mbali wa sekta zinazosimamiwa na Kamati, pamoja na kukagua baadhi ya maeneo na miradi ya maendeleo ili kuona hatua na mafanikio ya utekelezaji wa sekta hizo ambazo zimefikiwa pamoja na kazi ya kupitia Miswada ya Sheria kwa kila Mkutano wa Baraza unapofanyika.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwatanabahisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ya kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi wa baadhi tu ya changamoto za Wizara na taasisi zake zinazoambatana na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati, hivyo maelezo zaidi na kwaukamilifu yanapatikana katika ripoti kamili ambayo tayari inaonekana katika "tablet zote za Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili.

**Mheshmiwa Spika,** Aidha, Kamati ilifanya kazi zake za mizunguuko mitatu (3) kwa muda wa wiki Tisa (09) katika utaratibu iliojipangia kwa Unguja, Pemba na Tanzania Bara. Kadhalika, kupitia ripoti hii Kamati imeainisha changamoto zilizomo kwenye taasisi za umma na Idara Maalumu pamoja na kutoa maoni na ushauri wa kuzitatua changamoto hizo kwa kila Taasisi husika.

**Mheshmiwa Spika,** Kiujumla, Kamati imeridhishwa na kasi ya maendeleo ya Serikali ya Awamu ya Nane pamoja na utekelezaji bora wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa Taasisi zote ambazo zinasimamiwa na Kamati hii kutokana na juhudi kubwa wanazochukua katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kufuata miongozo na taratibu za nchi. Hivyo, mbali ya maoni, ushauri na

maelekezo yaliyotolewa kwa kila Sekta, Kamati pia inatoa maoni, ushauri na maelekezo ya jumla kwa Taasisi hizo kama ifuatavyo:

## 2.1 Ofisi ya Rais Ikulu

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inatoa pongezi za dhati kabisa kwa Ofisi hii kutokana na mafanikio mbali mbali yaliyopatikana katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti yake kwa mwaka 2022/2023 sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025. Aidha, Kamati imeridhishwa na namna Ofisi hii inavyozisimamia Taasisi za Umma katika kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Hussein Ali Mwinyi pamoja na viongozi wengine wakuu wa nchi.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kupitia Taasisi ya Nyaraka kuzidisha mashirikiano na Taasisi za Umma na Binafsi kwa lengo la kuimarisha mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu na kutunza historia ya Zanzibar. Aidha, Kamati inaishauri Taasisi hii kujenga mashirikiano ya karibu na Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweka mifumo bora ya kielektroniki katika kuhifadhi na kulinda Nyaraka kwa njia za kisasa.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati vile vile, inaishauri Serikali kuendeleza mpango wa ujenzi wa jengo jipya la Nyaraka katika eneo la Kilimani baada ya kukamilika kwa mpango wa manunuzi ya nyumba mbili zilizokaribu na ofisi hii.

**Mheshmiwa Spika,** Aidha, Kamati inashauri mpango wa mradi unaoandaliwa wa ujenzi wa jengo jipya la Nyaraka kufanywa kwa haraka na kuwashirikisha wataalamu wa pande zote mbili za Muungano ili kupata ushauri wa kitaalamu na wa kifedha wa

masuala ya uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kwa kufuata utaratibu na miongozo ya nchi yetu.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati imesikitishwa na kuona zipo baadhi ya Taasisi ambazo hazitekelezi kwa vitendo Miongozo na mafunzo ya Utunzaji na Udhibiti wa Siri za Serikali yanayotolewa na GSO katika utendaji wao wa kazi wa kila siku. Hivyo, Kamati inazitaka taasisi husika kuwachukulia hatua watumishi wote wanaokaidi miongozo hiyo kwa vitendo ili kujenga mustakbali uliobora kwa Taifa lakini kwa maendeleo ya Utumishi wa Umma.

## 2.2 Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

**Mheshmiwa Spika,** Ofisi hii pamoja na kusimamia idara mbalimbali, inajukumu pia la kusimamia na kuratibu Ofisi ya faragha ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na masuala ya Sera, Mipango na Tafiti za Ofisi.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inaipongeza Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwa kuvuka malengo katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na ada ya uhifadhi na ukaguzi wa Mazingira kwa upande wa Unguja, ambapo katika kipindi cha Julai – Septemba 2022 walifikia asilimia 112%. Aidha, Kamati inashauri mafanikio haya pia yasimamiwe kwa upande wa Pemba ili kwenda sambamba na malengo ya Mamlaka katika ukusanyaji wa mapato.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati pia, inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kutekeleza vyema miradi ya uhifadhi wa mazingira katika maeneo ya Tovuni Wilaya ya Wete, Sipwese Wilaya ya Mkoani na Likoni katika Wilaya ya Wete. Vile vile, Kamati ilipata

fursa ya kufika Mkoni Mtwara katika fukwe ya Mikindani na kuona namna miradi kama hii inavyotekelezwa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kamati inashauri miradi kama hii pia ifanywe katika fukwe ya Kichanjaani katika Shehia ya Ndagoni Wilaya ya Chake – Chake kutokana na athari kubwa za kimazingira zinazoendelea kutokea.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika biashara ya Kaboni ambayo inachukua nafasi kubwa katika kuhifadhi mazingira. Jamii pia ishajihishwe kutumia nishati mbadala katika matumizi ya majumbani na kupanda miti kwa wingi kama ni njia mbadala ya kukabiliana na janga la mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshmiwa Spika,** Katika kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya Wizara itumie nguvu kubwa ya kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuwatunza na kuwalinda waathirika wa dawa za kulevya wakati wanapoacha kutumia dawa na kuwa wananchi wema katika jamii. Kamati imeona si busara kwa familia au jamii kuwatenga waraibu baada ya kuacha matumizi ya dawa za kulevya na kupata elimu kupitia Nyumba za Kurekebisha tabia ambazo zinatumia fedha nyingi katika kuwakomboa vijana. Aidha, kwa upande wa Pemba Kamati inashauri kutafutwa eneo kwa ajili ya Kujenga nyumba ya Waraibu wa dawa za Kulevya ambayo itakuwa salama na kuepuka kukodi nyumba katikati ya makaazi ya watu.

**Mheshimiwa spika,** Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Hussein Ali Mwinyi kwa kumteuwa Ndugu Ussi Khamis Debe kuwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Watu wenye Ulemavu. Aidha, Kamati

inaipongeza Ofisi kwa kusimamia vyema programu ya Watu wenye Ulemavu na kuhakikisha wametekeleza majukumu yao kwa uweledi na ufanisi katika kuwahudumia watu wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa spika,** sambamba na hayo, Kamati imepata faraja sana kuona Idara hii imepata Sheria mpya ya Watu wenye Ulemavu (Haki na Fursa) Nam. 8 ya Mwaka 2022 ambayo imeweka wazi haki na fursa za Watu wenye Ulemavu katika jamii. Hata hivyo, Kamati inashauri kuiangalia Ofisi ya Baraza la taifa la watu Wenye Ulemavu Kisiwani Pemba kwa kuwatafutia Jengo lenye nafasi ya kutosha au kuwajengea Ofisi mpya kwa ajili ya utendaji bora wa kazi zao.

**Mheshmiwa Spika,** kwa upande wa Tuma ya Ukimwi, kamati inaishauri Serikali kuongeza program za kutoa elimu ya kujikinga na maradhi ya kuambukiza ikiwemo virusi vya HIV na UKIMWI kwani tumejenga mazoea ya kuwepo kwa magonjwa haya bila kuangalia athari zake zinavyozidi kuithiri jamii na Serikali kwa ujumla.

## 2.3 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

**Mheshmiwa Spika,** Jukumu la msingi la Wizara hii ni kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na masuala ya Muungano kwa upande wa Zanzibar. Mbali na kusimamia taasisi nyengine Ofisi hii pia, inasimamia Taasisi mbili zinazojitegemea ambazo ni Baraza la Wawakilishi la Zanzibar (BLW) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inashauri wizara kufuatilia na kusimamia kikamilifu taasisi za umma katika kutoa huduma zilizobora na

kuhakikisha kuwa miongozo na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inatekelezwa ipasavyo.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inasikitishwa na kitendo cha Taasisi za Umma kujenga tabia ya kutojibu barua za maombi au miongozo ambayo inatolewa kwa sekta za umma. Tabia hii inazifanya Taasisi za Serikali kukosa imani na wananchi wetu ambao tunawahudumia. Hivyo, Kamati inaishauri Ofisi hii kusimamia suala hili na kulitolea muongozo kwa mashirikiano na Tume za Utumishi ambazo ndio zenye wajibu wa kusimamia Utumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inachukua fursa hii kuzipongeza Serikali zote mbili, Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Dr. Samia Suluhu Hassan na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi kwa juhudi zao za kuhakikisha mradi huu unatekelezwa kwa ufanisi. Aidha shukurani za pekee zimfikie Mkurugenzi Mkuu wa TASAF, Ndugu Mwamanga kwa jitahada zake za kufanikisha mradi huu bila upendeleo wa upande wowote.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inachukua fursa hii pia, kuishauri Serikali kuzidisha kasi ya kusimamia utekelezaji wa miradi ya TASAF III ya ajira za muda mfupi na zenye tija ambazo zinaibuliwa na wananchi ambapo jumla ya Shehia 126 za mpango wa awali zimenufaika.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati katika mizunguuko yake ya ufatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti, imeridhishwa sana na utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya ujenzi wa kituo cha afya daraja la II (PHC+) katika

Shehia ya Uzi na ujenzi wa jengo la wazazi na kituo cha afya Vijibweni katika Shehia ya Donge Pwani ambapo kwa pamoja miradi hii ujenzi wake imeshafikia wastani wa asilimia 70. Kamati kwa upekee inashauri itakapokamilika miradi hii na itakapofika kuanza kazi kwa kituo cha Afya cha Uzi ajira za wafanyakazi wa Kituo hicho kupitia vigezo vinavyohitajika waangalie zaidi wazawa wa kisiwa hicho.

**Mheshmiwa Spika,** Aidha, Kamati inashauri kwa ile miradi mipya ambayo imepangwa kutekelezwa kwa mwaka huu na bado haijaanza, ni vyema Wizara kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa kwa wakati na kwa manufaa mapana ya wananchi.

**Mheshmiwa Spika,** Aidha, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba kutokana na juhudi zao za kutoa huduma kwa waheshimiwa wajumbe kwa kipindi chote cha Kamati zinapokua huko kwa ajili ya shughuli za utekelezaji wa bajeti za Wizara na Taasisi zake pamoja kutekeleza vyema majukumu yao ya kila siku chini ya uongozi wa Ndugu Abdulghani Abdalla Said, tunamuomba MwenyezMungu ampe uwezo zaidi wa kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo, katika maboresho ya Afisi ya Pemba, Kamati inashauri kusimamia kikamilifu matengenezo ya Ukumbi mkubwa wa mikutano ili kuweka mazingira bora ya utendaji na shughuli zote za Serikali zinazofanyika hapo.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inaitaka Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kushirikiana na wizara hii kuzidisha kasi ya kusimamia na kufuatilia haki na fursa za watendaji wa Baraza katika nyanja zote za kimaslahi ili kufanya kazi kwa weledi na ufanisi zaidi.

**Mheshmiwa Spika,** Vile vile, Kamati inashauri Afisi ya Baraza la Wawakilishi kuandaa mradi maalum wa ujenzi wa jengo jipya la ofisi, kumbi za Kamati ikiwemo ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili aweze kutekeleza majukumu yake akiwa Barazani, licha ya hayo kamati inaomba kushughulikiwa kwa maombi ya ununuaji wa gari za Ofisi pamoja na kwa ajili ya shughuli za kamati kwa kuwasilisha maombi Serikalini kwa haraka ili mradi huu upate kuombewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wake.

**Mheshmiwa Spika,** kwa upande mwengine, Kamati inashauri Afisi ya Baraza izidishe kasi ya kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watendaji wake ili kupata watendaji wenye uzoefu na wanaoendana na wakati na mazingira ya mabunge pamoja na kuweka uwiano bora wa maslahi kwa watumishi wa Baraza na Watendaji wengine wa Taasisi zinazojitegemea au kuangalia muundo wa maslahi kwa Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola.

## 2.4 Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora

**Mheshmiwa Spika,** Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imegawika katika sekta kuu tatu; ambazo ni Sekta ya Sheria, Sekta ya Uratibu wa Utumishi wa Umma na Sekta ya Utawala Bora.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati wakati ilipokua ikifuatilia taarifa za Wizara hii kupitia taasisi zake ilielezwa kwamba kumekuwa na upotevu wa majalada au taarifa muhimu za watumishi ikiwa pamoja na mikataba, aridhilhali, barua za vizuizi vya mishahara, vithibitisho vya kifo na barua za bodi ya madaktari. Kwa mantiki hio, Kamati inashauri kuchukuliwa hatua za haraka juu ya upotevu wa Majalada

au baadhi ya taarifa muhimu kwa baadhi ya wastaafu waliotumikia utumishi wao zaidi ya Taasisi moja katika Serikali na kukosekana kwa baadhi ya vielelezo muhimu katika majalada ya wastaafu.

**Mheshmiwa Spika,** kamati imeridhishwa na utendaji kazi wa Afisi ya mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali kwa utendaji wao na kuibadilisha ofisi kuwa ya kisasa zaidi. Aidha, Kamati inasikitishwa na kitendo cha ujazaji au uingizaji usioridhisha wa taarifa za mishahara katika Kalamazuu na kupelekea kukosekana kwa usahihi wa taarifa za hesabu za mafao kwa baadhi ya wastaafu. Kamati inashauri taasisi inayohusika kufanya ukaguzi wa suala hili ili taasisi zitakazobainika kuchukuliwa hatua za msaada.

**Mheshmiwa Spika,** kwaniaba ya wajumbe wa Kamati tunapenda kuishauri Serikali izitumie Taasisi za kusimamia haki jinai kutoa elimu juu ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na changamoto zake kwa kesi za udhalilishaji katika jamii na athari yake katika Nyanja za kiuchumi Kijamii na kisiasa kutokana na kundi kubwa la jamii kutofahamu maudhui ya Sheria na Haki Jinai inavyofanya kazi hapa Zanzibar.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati imebaini baadhi ya changamoto kadhaa ilipotembelea na kukagua eneo lenye kiwanja cha Chuo cha IPA kwa upande wa Pemba eneo la Mfikiwa. Kamati haikuridhishwa na eneo hili kwa ujenzi wa Chuo kutokana na mazingira yake kutokuwa rafiki, pamoja na fidia kubwa ya milioni 78 ambayo haiendani na vipando vilivyomo. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuzuia ujenzi ambao umepangwa kufanyika katika eneo hili na inapendekeza kutafuta

eneo jengine ambalo litaridhisha kwa ujenzi wa Chuo ambalo lipo salama lakini pia halitagharimu fedha nyingi kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaitaka Tume ya Utumishi Serikalini, kuweka utaratibu bora utakaoeleweka kwa waombaji wa ajira kwa kuweka wazi misingi na sababu zilizosababisha waomba ajira hao kukosa nafasi hizo za ajira ili kupunguza malalamiko yasiyo ya msingi.

## 2.5 Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi hiki kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Kamati imefanikiwa kutembelea na kukagua utekelezaji wa kazi za taasisi mbali mbali zilizochini ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini, Kamati imebaini kuwepo kwa malalamiko ya Waheshimiwa Madiwani pamoja na uongozi wa Baraza la Mji Kaskazini B na Serikali ya Wilaya kwa kutoridhika na ushirikiano wanaoupata kutoka Serikali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja hasa katika ugawaji wa fedha za maendeleo. Kamati haikufurahishwa na kitendo cha kutojaza nafasi ya Mwenyekiti mwengine wa Baraza tangu aondolewe madarakani aliyekuwepo kabla. Kamati inaitaka Wizara kuliingilia Kati masuala haya ili kuondosha malalamiko ambayo hayaleti sura nzuri kwa Baraza na wananchi wa Mkoa huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati wakati ikiendelea na ufuatiliaji na upokeaji wa taarifa za utekelezaji kwa robo ya pili katika Baraza la Mji Kati haikufurahishwa na uwepo kwa mgogoro wa kiutendaji na kimaslahi kwa Madiwani na Mkurugenzi wa Baraza la Mji kati. Hivyo, Kamati inaitaka Wizara kuingilia kati mgogoro huo wa kiuendeshaji baina ya madiwani na Mkurugenzi wa Baraza la Mji Kati ili kuondosha matabaka ambayo yameanza kujitokeza.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati haikuridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa vyoo vya skuli ya Maandalizi na Msingi ya Uchukuni na hivyo, inaliagiza Baraza kuhakikisha ujenzi huu unakamilishwa kwa wakati na kumsimamia mkandarasi kutimiza makubaliano ya mkataba.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuziagiza Mamlaka zinazohusika na kutoa mgawanyo wa fedha za maliasili na kuzipatia Mamlaka za Serikali za Mitaa fedha hizo kwa wakati ili kusaidia ukusanyaji wa mapato kwa Serikali za Mitaa na hivyo kuweza kutekeleza mipango yao ya maendeleo.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inashauri pia, Wizara kuandaa programu maalumu ya kutoa elimu ya kuwashawishi ipasavyo wafanyabiashara wadogo wadogo katika kuendeleza na kukuza biashara zao kwenye kila Halmashauri za Unguja na Pemba kwa lengo la kuyatumia vyema masoko ya wajasiriamali yaliyojengwa kila Wilaya Unguja na Pemba. Aidha, Kufuatia kukosekana kwa mapato ya kutosha kwa baadhi ya Halmashauri, Kamati inaagiza kila Halmashauri ifanye Mnada katika Halmashauri yao ili kusogeza huduma karibu na wananchi wao na kuongeza mapato kwa Halmashauri.

**Mheshmiwa Spika,** Kwa mwaka 2022/2023 Kamati ilipata nafasi ya kuyakagua milango ya wajasiriamali ambayo imejengwa katika maeneo mbali mbali Wilaya zetu; kamati imefurahishwa na uamuzi huo wa Serikali yetu ambao utawarahisisishia wajasiriamali kuendeleza biashara zao katika sehemu salama bila usumbufu wowote. Kamati inashauri Wizara kuzisimamia Serikali za Mikoa na kuhakikisha maeneo hayo wanapewa wafanyabiashara waliokusudiwa ili kuepusha maduka na vizimba vya masoko haya kumilikiwa na watu wasiokuwa walengwa na hivyo kuwanyima wahusika wake.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kuzisimamia Mamlaka husika katika utoaji wa leseni za biashara za vileo na kuweka utaratibu wa wazi na shirikishi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ukusanyaji wa mapato na utaratibu wa Matumizi kwa fedha zitokanazo na chanzo hiki cha mapato. Sambamba na hilo, Kamati inazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha wamezidisha nguvu ya kufanya usafi na ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri zote za Unguja na Pemba.

**Mheshmiwa Spika,** Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mradi wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vyuo vya Idara Maalum za SMZ ili kuweka mazingira bora ya kujifunzia kwa Maafisa na Wapiganaji wa Idara Maalum bila kuwepo kwa changamoto yoyote juu ya miundombinu na wataalamu wa mafunzo.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inapendekeza kwa Serikali kuunganisha nguvu za Idara Maalum na Mamlaka za Haki jinai katika kupiga vita matukio ya kihalifu katika jamii ambayo imepelekea kushamiri kwa vitendo hivi maeneo ya miji na vijijini kutokana na muingiliano mkubwa wa wageni na wenyeji wa maeneo haya.

**Mhesmiwa Spika,** Kamati katika utafiti wake wa muda mrefu na baada ya kutembelea Mahanga ya kisasa ambayo yamejengwa katika maeneo ya Muyuni na Kambi nyenginezo, imeona wazi kuwa kikosi cha Valantia (KVZ) kinaenda kuwa cha kupigiwa mfano kutokana na mafanikio yake ambayo yamepatikana kwa muda mfupi na hivyo utekelezaji wake kuweza kuridhisha chini ya Kamanda lutein Kanal Said Ali Shamhuna. Hivyo, Kamati kwa mara nyengine tena inapenda kuishauri Serikali Kuifanyia Marekebisho Sheria ya uanzishaji wa Kikosi cha Valantia (KVZ) ili kuweza kulinda kibiashara na kujipatia mapato badala ya kulinda Taasisi za Serikali.

**Mhesmiwa Spika,** Kamati pia, inaridhishwa na maendeleo mazuri yanayopatika kwa vikosi mbalimbali hapa nchini kwa wanavyotuma kutekeleza majukumu yao kiuledi, Kamati inatoa maoni kwa Serikali kutenga fungu maalum la mafuta kwa vyombo vya KMKM na KZU katika kutekeleza kazi zao za kila siku.

**Mhesmiwa Spika,** Kupitia Jeshi la kujenga Uchumi Kamati inashauri kuwapatia likizo zao za mwaka kwa wakati wapiganaji wake, kuwalipa fedha za likizo pamoja na kuhakikisha fedha za muda wa ziada (over time) kwa wapiganaji wanaofanya kazi katika muda wa ziada kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake.

**Mhesmiwa Spika,** kwa upande wa Kampuni ya Ujenzi ya Serikali Kamati inashauri Wizara kuiangalia kwa jicho la karibu Kampuni hii na kupewa kazi wanazostahiki badala ya kazi nyingi kupitia moja kwa moja katika vikosi. Aidha, Kamati yangu inazitaka Taasisi ambazo zinazodaiwa na Kampuni ya Ujenzi wa Serikali ikiwemo JKU na ZURA kuharakisha malipo yao haraka iwezekanavyo. Sambamba

na hilo, Kamati inashauri kuwatafutia Kampuni hiyo jengo jengine kwa ajili ya kuendeleza kazi zao za Ofisi kwakuwa sehemu waliopo sasa sio rafiki kwa utendaji kazi zao;

## 3. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla Kamati yetu inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Taasisi zote ambazo zipo chini ya Kamati hii kutokana na mashirikiano yao makubwa tunayopata kutoka kwa viongozi wa Taasisi hizo, akiwemo Mhe. Jamal Kassim Ali; Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu. Mhe. Harous Said Suleiman; Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Hamza Hassan Juma; Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Mhe. Mwalim Haroun Ali Suleiman; Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, pamoja na Mhe. Masoud Ali Mohammed; Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ,

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaomba kuwashukuru Makatibu wakuu na Wakurugenzi wote wa Taasisi hizi, Makamanda wa Idara Maalum, wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wote wa Zanzibar na Makamishna kwa ushirikiano wao mkubwa walioipatia Kamati wakati wa kazi zake. Aidha, Kamati inawashukuru watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar wakiongozwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Ndugu Raya Issa Mselem pamoja Mkuu wa Idara ya Baraza la Wawakilishi Pemba ndugu Abdul-ghani Abdullah Said kwa ujasiri wao wa usimamizi na kuleta mabadiliko katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri viongozi wa Wizara na taasisi zote zinazosimamiwa na Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika mizunguuko ya ziara za

Kamati, kutokufanya hivyo kutaipelekea Kamati kushindwa kupokea taarifa zao kwa usahihi na zenye kuaminika mbele ya Kamati. Aidha, Kamati inaziomba Wizara zote na Idara zinazohusika kuyachukua maoni, ushauri na mapendekezo ya Ripoti kuu na yale yote yatayotokana na michango ya Wajumbe kwa kuyafanyia kazi na kuja kuyatolea ufafanuzi wa kuridhisha ikifika kikao cha mwezi wa Septemba kama Kanuni ya 109 (17) ya Baraza la Wawakilishi, toleo la 2020 inavyoelekeza .

**Mwisho Kabisa**, kwa kumalizia, napenda nikushukuru tena Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii na pia, niwaombe Waheshimiwa wajumbe wa Baraza hili Tukufu kuisoma, kuifahamu na kuichangia Ripoti hii kwa umakini mkubwa.

**Mheshimiwa Spika, *Naomba Kutoa Hoja.***

Ahsante,

……………………………………

**(Machano Othman Said)**

**Mwenyekiti;**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**<u>ZANZIBAR</u>**